

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO  
SHULE YA SEKONDARI TUNUNGUO

S.L.P 23

NGERENGERE Simu:-0739221424

Au 073970691726/12/2020

Kumb.Na.TUSS/J/21

Jina la Mwanafunzi.....

S.L.P .....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TUNUNGUO  
MWAKA 2021

1.0 . Utangulizi:

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha I, katika shule hii mwaka 2019. Shule ya Sekondari Tununguo (**SHULE NI YA KUTWA**) ipo umbali wa km 200 Kusini Mashariki mwa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro. Usafiri wa basi kutoka Mjini Morogoro unapatikana katika kituo cha mabasi cha MSAMVU, nauli Tshs.10000/= nakutoka Dar es Salaam mabasi yanapatikana BUGURUNI na UBUNGO TERMINAL , nauli Tshs 12,000/=.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 21/01/2021 (ndani ya siku kumi).

2.0 . Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 . Sare za Shule

a) Sare ya shule hii ni suruali kwa wavulana na sketi kwa wasichana na Shati nyeupe. [Rangi ya kitambaa cha sketi na suruali ni maruni/ damu ya mzee], pea mbili na viatu rangi nyeusi jozi mbili. Hijab rangi nyeupe.

b).Sare ya michezo kwa shule hii ni bukta nyeusi na flana ya bluu kwa wavulana na sketi nyeusi na flana ya bluu kwa wasicha na na raba nyeupe jozi moja.

2.2 .Daftari, kalamu, School bag na Mkebe wa hesabu

2.3 .Jembe, panga kwa wavulana, kwanja na jembe kwa wasichana na fagio pamoja na ndoo ndogo kwa wote.

**3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria za Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebisha kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia,yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni ijambo la lazima. b.Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;

- c.Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
- d.Kuwahi Katika kila shughuli ya shule na nyingine utakazo pewa;
- e.Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- f.Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- g.Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- h.Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- i.Kutunza mali za shule

### **3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABAISHA KUFUKUZA NA KUSIMAMISHWA SHULE:-**

- a.Wizi
- b.Uasharati na ushoga
- c.Ubakaji
- d.Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubelin.k.
- e.Kupigana na kupiga
- f.Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g.Kudharau bendera ya Taifa
- h.Kuwa mjamzito/Kupa tamimba
- i.Kuo au kuolewa
- j.Kutoa mimba
- k.Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- l.Kukataa adhabu kwa makusudi
- m. Kuwa na simu ya mkononi

### **4:0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

- a. Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c.Fomu ya mzazi kukiri na kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

Tanbihi

**Tafadhali soma kwamakinimaelezo/maagizohaya**

**Nakuyatekelezakikamilifu.**

“Karibu sana katika shule hii”

.....  
 MKUU WA SHUL  
 THE HEADMASTER  
 TUNUNGUO SECONDARY SCHOOL